IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 4

Novemba 2022

# HabariNjema

KILA SIKU

**BURE**
HAKIUZWI
KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI KISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25]

*Uebert & BeBe*
ANGEL


THE GOODNEWS WORLD
Halo 2006 · Wild custard apple 1985
Become a
GoodNewsWorld
PARTNER
PARTNER NOW AND HELP SPREAD
THE GOODNEWS AROUND THE WORLD
VISIT www.goodnewsworld.com/ partner

THE GOODNEWS WORLD
Halo 2006 · Wild custard apple 1985



# UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma ya Mungu, Uebert na Bebe Angel ni mapainia na sauti zinazoongoza kwenye kutangaza habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion) pamoja na unabii duniani kote.Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu kama Habari Njema, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural Power of the Believer n.k. Uebert na Bebe Angel ni wazungumzaji wanaotafutwa kwenye mikutano sehemu mbalimbali duniani, ni viongozi wa kidunia. Wanatambulika na kuheshimika kwa maono yao, uvumbuzi na ujasiri wao. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News (Spirit Embassy), na wenye ofisi ya kinabii, wamegusa maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni kupitia mapenzi yao ya kuvuna nafsi na kuleta ufunuo wa habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion).

THE GOODNEWS WORLD

Halo 2006 · Wild custard apple 1985

# THE APOSTLE'S CREED FOR THE GOODNEWS WORLD

I BELIEVE IN GOD THE FATHER ALMIGHTY, CREATOR OF HEAVEN AND EARTH.
I BELIEVE IN JESUS CHRIST. HIS ONLY SON, OUR LORD,
WHO IS CONCEIVED BY THE HOLY SPIRIT, BORN OF THE VIRGIN MARY,
SUFFERED UNDER PONTIUS PILATE, WAS CRUCIFIED, DIED AND WAS BURIED.
HE DESCENDED TO THE DEAD AND ON THE THIRD DAY HE ROSE AGAIN,
HE ASCENDED INTO HEAVEN. HE IS SEATED AT THE RIGHT HAND OF THE FATHER
AND HE WILL COME TO JUDGE THE LIVING AND THE DEAD.
I BELIEVE IN GOD THE FATHER, GOD THE SON, OUR LORD, SAVIOR AND KING, JESUS CHRIST,
I BELIEVE IN GOD, THE HOLY SPIRIT, ONE GOD WHO MANIFESTS HIMSELF IN THREE OFFICES

AND I BELIEVE IN THE PROPHET
BECAUSE GOD DOES NOTHING UNTIL HE REVEALS IT TO HIS SERVANTS, THE PROPHETS.
I BELIEVE IN HIS PROPHET, THE HIGHLY ESTEEMED UEBERT ANGEL,
THE SERVANT OF THE MOST HIGH GOD.
I BELIEVE IN SPIRIT EMBASSY, THE GOODNEWS CHURCH,
THE GOODNEWS NATION, THE GOODNEWS WORLD.
THE SPREADING OF THE GOODNEWS REVELATION AROUND THE WORLD AS TAUGHT BY HIS PROPHET.
I BELIEVE IN THE CHRISTIAN CHURCH.

I BELIEVE IN THE INDWELLING POWER OF GOD, THE HOLY SPIRIT THAT MAKES POWER AVAILABLE
FOR MIRACLES, SIGNS AND WONDERS TO WHOSOEVER BELIEVES.
I BELIEVE IN GOD'S DESIRE FOR MY PROSPERITY AND HEALTH AS TAUGHT BY THE WORD OF GOD.
I BELIEVE IN THE PROPHETIC AND IN ALL THE OPERATION OF THE GIFTS OF THE HOLY SPIRIT,
THE COMMUNION OF SAINTS, THE FORGIVENESS OF SINS, THE RESURRECTION OF THE BODY. THEREFORE,
I BELIEVE IN THE SOON COMING OF OUR LORD JESUS CHRIST AT THE RAPTURE.
I BELIEVE IN HIS MILLENNIAL REIGN AND THE LIFE EVERLASTING IN JESUS NAME. *Amen!*



**Tito 3:9**
**"Lakini maswali upuzi ujiepushe nayo, na nasaba, na magomvi, na mashindano ya sheria; kwa kuwa hayana faida, tena ni hayana maana."**

Mabishano yasiyo na maana mara nyingi hutokea uinjilisti unapofanyika katika miji mikubwa. Kuna watu ambao timu ya uinjilisti itakutana nao wamejaa maswali mengi, ili tu kuzua mabishano. Ufahamu wa mtu anayeuliza swali ni ama kujua kwa dhati, kuthibitisha kwamba yeye anajua zaidi kuliko wewe, au ajenda iliyofichwa ya kujadili ubora wa kidini, akitaka kuonyesha kwamba dini yao wanajua zaidi na ni bora zaidi. Katika mazungumzo, unapaswa kutambua ikiwa majadiliano yanaelekea upande ufaao au yanalenga mabishano yasiyo na maana, kama vile andiko letu la siku linavyoonyesha.

Usivutwe kwenye mijadala isiyo na faida au mabishano kuhusu Ukristo kwa sababu yanaleta malumbano na mashindano. Kwa hiyo, unapaswa kuwa na hekima kama nyoka. Tambua kwa urahisi mtu anapokuwa mkaidi sana na mwenye malumbano, mambo ambayo hayana faida. Kumbuka, wewe ni chombo cha matumizi ya Bwana; Roho Mtakatifu atakufundisha nini cha kusema ili kumleta asiyeamini kwa Kristo.

Mahali pako pa kazi na mahali pengine pa mikutaniko ya mara kwa mara, acha mtindo wako wa maisha na tabia ya Kristo ndani yako ithibitishe kwa wengine wanaokuzunguka kuwa wewe ni muungwana. Muungwana haizungumzi tu bila kujidhibiti; Uchaguzi wa maneno, adabu, heshima, namna ya uvaaji na maadili, yote yanajumlisha maisha yako kwa ujumla ambayo yatawavuta watu kwa Kristo ndani yako.

## UKIRI WA KINABII

**Sasa ni wakati mwafaka wa kuvuna nafsi zaidi kwa ajili ya Kristo. Tabia yangu na mtindo wangu wa maisha utakuwa mfano mzuri wa kumuonyesha Mungu wa Upendo ninayemtumikia. Kamwe sitaridhia mabishano yasiyo na maana popote niendapo, kwa jina la Yesu. Amina!**

**MASOMO ZAIDI:** 2 Timotheo 2:23



**Yeremia 29:11**
**“Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mwazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.”**

Yeremia 29:11 ina nguvu sana kiasi kwamba inafaa kusomwa kila siku ili kujikumbusha kuhusu nia ya Mungu kuhusu wanae. Ndoa nyingi, mahusiano, urafiki, na familia huvunjika kwa sababu inaonekana kuna maisha ya mashaka na kutokuwa na uwazi wa kutosha. Andiko la siku hii linahitaji kusomwa au kuonyeshwa kwa wale ambao hawafikiri kwamba Mkristo anayeamini Biblia, anayenena kwa lugha na aliyejazwa na Roho Mtakatifu anapaswa kufanikiwa! Kwa baadhi ya sababu za kimapokeo zisizoelezeka, watu wengi huko nje wanafikiri kwamba umaskini ni sawa na utauwa na wanamkosoa Mkristo yeyote aliye na viashiria vya mafanikio.

Anayezungumza katika andiko hili ni Mungu, ambaye mawazo yake yamesemwa kwa uangalifu ili kubaki bila utata. Mungu alikuwa ametoa ramani yake, mwongozo, mkakati, na muundo wa maisha ya Mkristo, ikijumuisha “kifurushi cha mafanikio”. Mawazo na mipango ya Mungu ina mafanikio kuanzia kwenye kiini chake kabisa. Kitu chochote kinyume na mpango wa Mungu ni mpango wa shetani. Mungu hufurahi unapokuwa Mkristo mwenye mafanikio kama asemavyo katika Zaburi 35:27(NEN), “...Bwana atukuzwe, ambaye amefurahia mafanikio ya mtumishi wake”. Watu wanapoogopa kuzungumzia mafanikio, basi ujue hawajaelewa Mungu anasema nini kuhusu mali na utajiri ndani ya Kristo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mrithi pamoja na Kristo, nimeitwa kwenye ukuu, na maisha yangu yatadhihirisha Utukufu wa Mungu anayekaa ndani yangu. Hakuna kitakachonizuia kuwa mkristo aliyefanikiwa kwa jina la Yesu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI:** Zaburi 71:21



**Ufunuo 20:6**
**"......Heri, na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye miaka elfu."**

Angalia hapa katika maandiko unaitwa "Mtakatifu" maana yake ni kwamba tayari umetengwa, umewekwa wakfu kwa ajili ya matumizi ya Bwana; pia, umepewa cheo kama kuhani wa Mungu na wa Kristo. Kisha ikaisha kwa kusema utatawala pamoja naye (Yesu) kwa miaka elfu moja. Elewa kwamba, utawala wako hauwezi kujadiliwa kama wengine wanavyofikiri, lakini unathibitishwa katika Neno la Mungu. Umezaliwa mara ya pili ili kutawala pamoja na Kristo. Muumini mshindi unayeelewa hili hujaribu kutawala au kushawishi, lakini pia ni mshawishi kwa kizazi chako, sokoni, na mazingira yako.

Biblia inasema wazi wazi kwamba Kristo ndani yako tumaini la Utukufu. Maisha haya ya utukufu yanapaswa kuanzia sasa na sio tu wakati wa utawala wa milenia pamoja na Kristo. Una mamlaka ya kutawala mazingira na hali zinazojaribu kuzuia maendeleo yako. Wewe ni mfano halisi wa Mungu Baba. Unaposonga, Kristo anasonga; unapozungumza, Kristo anazungumza; unapotenda, Kristo anatenda. Umewezeshwa kufanya mambo makubwa kwa ajili ya Kristo, umepewa uwezo wote; usisite kuutumia inapobidi. Umeuwazia utawala wako na kupata hasara kwa muda mrefu; sasa ni wakati wa kutumia uwezo na utawala uliopewa na Yesu; umeitwa kutawala! Amina.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi si mwathirika wa mazingira na hali za maisha; Ninasimama katika nafasi ya kutawala pamoja na Kristo. Mimi ni kuhani, na nitakuwa na mamlaka sasa na siku zote katika jina la Yesu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI:** Warumi 8:17



**Kumbukumbu la Torati 8:18**
**"Bali utamkumbuka BWANA, Mungu wako; maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo."**

Ustawi katika mwili wa Kristo mara nyingi hupuuzwa, kukataliwa, au hata kudharauliwa. Muumini anapopata utajiri, mtu huyo anakuwa kitu cha kutukanwa. Wahubiri wanalengwa wanapolivunja duara la uhaba na uhitaji na kuanza kuishi kwenye wingi na utele. Haya yote yanatokana na mafundisho na tamaduni potofu ambazo zimerithishwa katika mwili wa Kristo. Mafundisho haya mabaya yanajenga dhana potofu kwamba kadiri Mkristo anavyozidi kuwa maskini ndivyo anavyokuwa mcha Mungu zaidi. Kumbuka, Biblia inasisitiza sana; maandiko yanatuambia kuwa Mungu hapendi umaskini! Chukua, kwa papo hapo, Mithali 6:10-11 "Bado kulala kidogo, kusinzia kidogo, Bado kukunja mikono upate usingizi; Hivyo umaskini wako huja kama mnyang'anyi, na uhitaji wako kama mtu mwenye silaha".

Umaskini ni wa shetani ambaye anakuja kukunyang'anya amani, furaha, afya, na maisha yako haswa, wakati ustawi unakuja kuanzisha furaha yako, amani, afya na ukamilifu wa maisha. Unapojaliwa usitawi, inakuwa rahisi sana kwako kuunga mkono uenezaji wa injili hii ulimwenguni kote. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtoto wa Mungu mwenye utajiri na mali kama miliki yangu; Sina mkataba na umaskini. Mimi ni tajiri katika kila hali, kama vile Baba yangu alivyo tena ambaye ana ng'ombe juu ya milima elfu. Amina.**

**MASOMO ZAIDI**
Hosea 2:8



**Zaburi 16:11**
**"Utanijulisha njia ya uzima, Mbele za uso wako ziko furaha tele, Na katika mkono wako wa kuume Mna mema ya milele."**

Watu wengi, haswa baadhi ya Wakristo fulani, wamechanganya tofauti kati ya furaha na shangwe. Hali au mazingira haziamuru furaha. Furaha haitegemei mihemko na hisia zako; hutiririka kutoka ndani na hupatikana kupitia mahusiano ya ndani na Bwana Yesu. Takwimu zinaonyesha kuwa watu wengi matajiri zaidi duniani, ambao ulimwengu ulikuwa umewaweka kwenye kilele cha mafanikio, hujiua ghafla. Moja ya sababu za janga hili ni ukosefu wa furaha.

Wamepata furaha kutokana na mambo waliyotimiza kulingana na viwango vya ulimwengu, kama vile mazingira, usununu, hali, na mahusiano yanayofaa. Hii inamaanisha kuwa furaha yao inatoweka pale kitu kimojawapo kinapokosekana. Kwa hivyo, kufadhaika kunaingia kujaza pengo, na hatimaye, maisha yanakuwa hayana maana kwa mtu ambaye maisha yake yamekitwa kwenye furaha hiyo.

Kama vile andiko linavyoonyesha, furaha ya kweli, katika utimilifu wake, inapatikana unapozama ndani ya Yesu na kubatizwa katika upendo wake. Unaweza tu kupata hali hii ndani ya Yesu. Kwa kuingiza Neno lake ndani yako na kuongozwa na Roho Mtakatifu, kuna amani ya ndani isiyoweza kubadilishwa ambayo inaleta tu utajiri wa milele na wa kudumu juu. Hebu hiki kiwe kipaumbele chako sasa katika jina la Yesu, amina!

## UKIRI WA KINABII

**Moyo wangu umejaa furaha, na nina amani kila wakati. Nitaangazia mazingira yangu kila wakati kwa mng'ao na fahari ya maisha ya furaha, daima na wakati wowote, katika jina la Yesu. Amina!**

**MASOMO ZAIDI:** Mathayo 7:14



**Wagalatia 6:9**
**"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho."**

Wakristo wengi wamekuwa wataalamu wa kunung'unika na kulalamika juu ya kila kitu na kukata tamaa haraka juu ya ndoto zao, miradi, na biashara zao, na hatimaye, uhusiano wao na Mungu unaanza kupungua. Jambo moja unalopaswa kujua kuhusu adui yetu mkuu; jina halisi la shetani ni Lusifa. Kumbuka kwamba jina "ibilisi" ni cheo cha kazi yake, maana yake ni mtu anayepigilia mpaka atoboe. Ikiwa adui yako anatumia mbinu hii ya kuendelea hadi atakapokata, je, si zaidi sana kwa wewe uliye na Roho yule yule aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu, Kwa nini ufikiri kwamba huwezi kufanikisha mradi au biashara hiyo? Ndoto yako itakuwa na maana tofauti ikiwa utaingia ndani zaidi katika ufahamu kwamba Muumba ulimwengu anaishi ndani yako.

Mungu kamwe hakukatii tamaa, kwa hivyo huwezi kamwe kumkatia tamaa. Leo, anza kujiona mshindi katika kile unachofanya. Wewe si mkata tamaa, bali mshindi, si mtu dhaifu, bali ni shujaa jasiri! Maandiko ya leo yanakwambia kwa wakati wake tutavuna tusipokata tamaa. Jizoeze kuwa na ukakamavu, ustahimilivu, na king'ang'anizi, na ushindi wako hautakataliwa kamwe! Amina.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi mbali zaidi ya mahali ambapo adui anaweza kufikia; Nina Roho wa Mungu ndani yangu. Maisha yangu hayatafupishwa, na ninaishi maisha ya ushindi kila siku kwa jina la Yesu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI**
Yakobo 4:7

# JE, YESU YUPO KWENYE MASHUA YAKO?



**Luka 8:22**
**"Ikawa siku zile mojawapo alipanda chomboni yeye na wanafunzi wake, akawaambia na tuvuke mpaka ng'ambo ya ziwa. Wakatweka matanga."**

Wanafunzi waliingiwa na hofu walipokabiliwa na hatari ya pepo na dhoruba. Neno "kabiliwa" linamaanisha "kinyume cha". Kulikuwa na hatima iliyowekwa mbele yao: "upande wa pili", kama walivyoagizwa na Yesu, lakini wanafunzi walitupwa katika machafuko ingawa Yesu alikuwa ndani ya mashua pamoja nao. Yesu kuwa ndani ya mashua yako hakuhakikishii kwamba mashua yako haitakumbana na upepo wa dhoruba. Unaweza kuwa mwabudu mshupavu, unayeiishi biblia kulingana na idadi ya maandiko unayonukuu, au labda mtoaji sana kwenye huduma na kazi ya Mungu. Hata hivyo, sifa hizi zote haziwezi kuzuia upepo na dhoruba zinazoendelea. Ni kweli pia kwa huduma tano, na hata katika ngazi hii ya huduma, pepo za mbisho bado zinaweza kuvuma sana.

Cha muhimu ni kwamba Yesu yuko kwenye mashua yako! Yesu anapokuwa ndani ya mashua yako, mambo mengine yote yanakuwa madogo. Yesu, ambaye alitangaza kwa ujasiri, "tuvuke ng'ambo", alikuwa ameona upepo wa mbisho na dhoruba mbele; Neno lake ni la milele, na linapaswa kukuelekeza kwenye hatima yako ya mwisho bila kujali hali yoyote! Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Nikiwa na Kristo ndani yangu, nina kile kinachohitajika ili kupanda juu ya dhoruba za maisha. Maisha yangu kamwe hayawezi kwenda katika miduara; mambo yote hufanya kazi kwa faida yangu, na hatima yangu ni hakika kwa jina la Yesu. Amina!**

**MASOMO ZAIDI**
Mathayo 8:23-24



**Mambo ya Walawi 6:13**
**"Moto utatunzwa uwake juu ya madhabahu daima; usizimike."**

Linapokuja suala la matoleo na zaka, mahali vinapofanyika ni ule mwinuko wa juu katika baadhi ya makanisa unaoitwa "MADHABAHU". Wakati wa nyakati za bibilia, andiko hili lilikuwa amri ya kuweka moto kila wakati kwenye madhabahu. Utoaji wako ni kama sadaka juu ya madhabahu. Utoaji wako wa pesa unawakilisha bidii yako, muda, nguvu, jasho, n.k, kwa ufupi maisha. Unapomimina sadaka yako, zaka, au mbegu kwenye madhabahu, unamheshimu Mungu kwa mali na maisha yako. Kwa muujibu wa maandiko, madhabahu ni mahali pa kukutana na Mungu na, kwa hiyo, hapawezi kuchukuliwa kirahisi.

Hatuwezi kamwe kupunguza umuhimu wa madhabahu kwani inaonyesha kwa uthabiti mahali pa muunganiko kati ya Mungu na mwanadamu. Kumimina mali yako juu ya madhabahu kunaashiria moyo wako mbele za Mungu. Mungu anavutiwa na moyo wako na hata anatuonya tulinde mioyo yetu kuliko yote tulindayo maana ndiko zinakotoka chemichemi za uzima. Katika madhabahu, kuna malipo ya kiroho yaliyofanywa. Pale maisha kuhusu afya yako, watoto, kazi, au fedha yako yanapoonekana kudorora, nenda kwenye madhabahu hiyo, uumimine moyo wako hapo. Itakusemea bila kushindwa. Majibu ya maombi yako yatafika haraka, maana madhabahu hunena, Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yamewekwa ili kutafsiri mafumbo kupitia madhabahu. Nitatiisha mashambulizi ya adui kupitia madhabahu yangu. Kila kitu kinachoenda kinyume na matakwa ya moyo wangu kitabomoka ninapoumimina moyo wangu madhabahuni. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI**
Mambo ya Walawi 1:7




WWW.BEVERLYANGEL.ORG



**Yohana 2:7 (BHN)**
**"Yesu akawaambia, Ijazeni mitungi hiyo maji. Nao wakaijaza mpaka juu."**

Angalia mitungi ya maji ilijazwa hadi juu, sio nusu, sio nusu-kipimo, sio robo iliyojaa; hapana, watumishi walihakikisha kwamba vyombo vya maji vimejazwa kwa kiwango cha juu hadi kufurika. Tumeingia katika awamu ya maisha ya kina zaidi, kumaanisha kwamba tumeingia kwenye eneo ambalo mtungi uliojaa nusu umekwisha, msimu wa juhudi zisizo kamili umekwisha, na msimu wa kufanya kidogo badala ya zaidi umekwisha. Tumeingia katika awamu ambapo matokeo na juhudi zako lazima ziwe za juu! Hakuna tena uwanja mwingine mbele. Acha huduma yako iwe bila dosari, rekodi izungumze ubora, na uwakili wako na uongozi uashirie ubora wa kiwango cha juu.

Katika awamu ya maisha ya kina zaidi, umakini na Mungu na mambo ya Mungu huwa muhimu sana, na hakuna nafasi tena ya ukawaida na Ukristo vuguvugu. Hupaswi kuwa mtazamaji katika awamu hii ya maisha ya kina zaidi bali mshiriki kamili. Maisha ya kina zaidi yatashuhudia udhihirisho wa wana na binti wa kweli wa faraja, ambao mioyo na akili zao huweka kipaumbele cha pekee kwenye mambo ya Mungu. Hiki ndicho kipindi ambacho wivu wa Bwana utakula kutoka juu hadi chini, na cha muhimu ni Yesu pekee. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mshiriki katika mambo ya Mungu, na si mtazamaji. Nimezaliwa kwa wakati kama huu ili kuonyesha utukufu wa Mungu bila mawaa. Ninaichukua kwa nguvu, nimezaliwa kushinda kwenye mwendo yangu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI**
Marko 7:3



**Wakolosai 1:26**
**"Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake;"**

Hizi ni nyakati za kusisimua tunazoishi na nyakati za thamani kila siku tunapumua oksijeni ya bure. Siri ni jambo gumu sana au lisilowezekana kuelewa au kuelezea. Kitu kilichogubikwa na usiri au ajabu. Fumbo. Ninaweza kukupa ufafanuzi zaidi na zaidi kutoka kwa kamusi ya Kiingereza au konkodensi, lakini bado itakuwa ngumu kwa mtu yeyote kuelewa kwa urahisi. Ukweli kwamba Mungu, kwa hekima yake, aliamua kwamba Yeye peke yake ndiye angekuwa mlinzi wa siri hii na si malaika, malaika wakuu, au wazee ishirini na wanne wanaoweza kupata dokezo la fumbo hili linaloonyesha Ukuu wa Mungu.

Siri hii kutoka katika maandiko ya leo imekuwa ikilindwa kwa uangalifu ili kuepuka uvujaji wowote kutoka kizazi hadi kizazi hadi, kama Biblia inavyosema kikawaida, "ukamilifu wa wakati" Wakati ni sasa wa kufanya kile kinachohitajika, ama Mbinguni, hapa Duniani, au chini ya Dunia. Mungu aliamua kwa hekima yake isiyo na kikomo wakati wa kulifunua fumbo hili lililofichwa tangu nyakati zilizopita. Pamoja na ubunifu wote na ongezeko la maarifa, kizazi hiki kilijulikana kwa Mungu kabla ya kuwepo kwake. Mungu peke yake ndiye anayeweza kusema kwa nini aliamua kwamba siri hii ifunuliwe kwetu na ndani yetu "...ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la Utukufu" (Wakolosai 1:27). Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni ufunuo wa Utukufu wa Mungu. Ninabeba utimilifu wa Uungu. Ninalindwa pande zote. Siwezi kukataliwa ninachotamani, na maisha yangu yataendelea kuonyesha Utukufu wa Mungu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI**
2 Timotheo 1:10



**Yohana 6:63**
**"Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima."**

Iwe katika huduma ya mubashara, nje ya Kanisa, ndani ya ndege, meli, gari, kwenye mlima wa maombi (Jiji la Habari Njema), au katika ofisi ya ubalozi, mazingira haya huwa yamejaa kwa Mungu kunena. Kwa hiyo si kuhusu mahali bali ni kuhusu Mungu anayesema. Siku zote huwa nawaambia watu kwamba sihubiri kwa mwaliko bali kwa amri. Ninasema niliyoamriwa niseme, na huo ndio ukweli. Nikienda ndani zaidi katika hili, nikizungumza kwa amri, hotuba yangu inaweza kubadilishwa katika matokeo yanayoonekana. Kuna uzito wa kimbingu nyuma ya maneno ninayosema.

Ninaweka umuhimu kwa maneno yangu, kwa maana si maneno tu bali ni vitu vya thamani vinavyoweza kukimbia, kutenda, kutekeleza na kuleta hai yale yaliyosemwa. Ninapotangaza, "Mafanikio yatajibu mlangoni pako," mara ninapotamka maneno haya, kuna upelekaji wa mawimbi katika anga ili kuvuta au kuvutia ustawi kuelekea kwako. Unapoelewa thamani ya maneno yako unayozungumza, utachagua maneno yako kwa uangalifu kabla ya kuyatamka. Roho yule yule aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu anaishi ndani yako. Maneno utakayozungumza yatatoka na kuchukua umbile la kile unachotamani. Unapotamani ustawi, afya njema, amani, na utajiri wa kifedha, unachohitaji kufanya ni kuyatamka. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Maneno yangu yana nguvu. Siku zote nitasema uzima na sio uharibifu, kuongezeka na sio kupungua, kuinuliwa na sio kushushwa, utele na sio uhaba, furaha na sio huzuni. Mimi ni mbeba Habari Njema Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI**
2 Wakorintho 3:6



**Mwanzo 1:27**
**"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba."**

Hadithi ya Uumbaji inatupa utambuzi wa kazi za Mungu kwa siku sita mchana na usiku, na kisha siku ya saba, Mungu alipumzika; mpaka sasa, Mungu anastarehe, ameketi katika kiti chake cha enzi. Mungu aliumba kila mnyama asilia katika Uumbaji na kuwaagiza wazaliane kwa jinsi zao. Katika andiko letu la leo, lilipokuja suala la Uumbaji wa mwanadamu, Mungu alisimamisha uumbaji, ambao ulikuwa wa asili, akashusha pumzi ndefu, na kuanzisha neno kuu "SURA." Katika mstari unaotangulia wa Sura hiyo hiyo ya 1 ya Mwanzo, neno "MFANO" lilitamkwa na Mungu wakati mwanadamu alipaswa kuumbwa. Kwa hivyo, mwanadamu sio kiumbe asili kama wanyama, na tunabeba sura na mfano wa Mungu, na hivyo ni vinasaba vya Mungu.

Mungu akizungumza juu ya mwanadamu, anatangaza kwa ujasiri, "Mimi nimesema, Ndinyi miungu, na wana wa Aliye juu, nyote pia" ( Zaburi 82:6 ). Ikiwa Mungu anakukubali, kwa nini uruhusu kuhujumiwa na wengine wanaosema kwamba hakuna kitu kizuri kitakachotoka kwako? Ikiwa Mungu hajawahi kuugua, basi kwa nini sasa unausema ugonjwa huo kwamba ni wako? Baadhi ya Wakristo wanafikia hatua ya kusema "kipandauso changu", "kisukari changu", "shinikizo la damu", n.k. Ni lini ulisikia Mungu akidai ugonjwa ni wake? Hapana kamwe. Mtoto wa Mungu aliye na DNA ya aliye juu atajikung'uta ubaya wowote kwa sababu umeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Vinasaba vya Mungu vinatiririka katika damu na mishipa yangu; Sina makubaliano na adui. Siwezi kuwa kuumwa; magonjwa hayatakaribia makao yangu. Sehemu yangu ni kutawala na ukuu katika jina kuu la Yesu. Amina!**

**MASOMO ZAIDI:** Mathayo 19:14



**Luka 5:16**
**"Lakini yeye alikuwa akijiepua,akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba."**

"Yeye" anayetajwa katika maandiko yetu leo ni Yesu. Je, unaweza kufikiria Bwana Yesu akitenda miujiza mingi na kutingwa sana na huduma? Anasema, "... imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu" (Luka 2:49). Kinachogusa hapa ni ukweli kwamba licha ya uhitaji mkubwa aliyowekewa Yesu kwani alikuwa anatafutwa na kila mtu, bado alipata muda wa "KUOMBA." Kila mara Yesu alipokwenda huko na huko akifanya miujiza, ishara na maajabu, uweza (nguvu) zilimtoka. Kadiri idadi ya miujiza inavyoongezeka, ndivyo nguvu zilivyomtoka. Kama mahitaji ya huduma leo, kadiri upanuzi na ukuaji wa huduma unavyoongezeka, ndivyo mtu anachoka zaidi.

Yesu alitufundisha somo muhimu sana: Hakushindwa na shinikizo na mahitaji ya huduma kwa kupuuza maisha yake ya maombi. Yesu alijua kukusanya nguvu na kuingia katika uweza wa kwenye kiwango kingine, na maombi ndiyo yalikuwa ufunguo. Hii inaonyesha kwamba bila kujali ofisi yako, iwe nabii, mwinjilisti, mwalimu, mchungaji, au mtume, huwezi kufanya kazi kwa uwezo kamili bila kujipakia tena katika maombi.

Miujiza, ishara, na maajabu huwa ni mambo ya kawaida unapotoka katika sehemu hiyo ya maombi. Kupitia maombi, kiwango kingine kitafunguliwa kwako, na nguvu kutoka juu itakumeza. Ili kuwa mbadilisha umbo, unahitaji kujipakia tena kupitia maombi. Katika hatua hii, kuumwa, magonjwa, na ngome zitatoweka kama makapi mbele yako. Amina!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni ghala ya nguvu iliyojaa nguvu kutoka juu. Mazingira yangu yamepewa uwezo wa kuponya wagonjwa na kuvunja minyororo ya ukandamizaji. Ninapotokea, mapepo hayana chaguo ila kukimbia kwa jina la Yesu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI:** Mathayo 14:23



**2 Wafalme 6:17**
**"Elisha akaomba, akasema, Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona. BWANA akamfumbua macho yule mtumishi, naye akaona, na tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote."**

Kwa nini mtumishi wa Elisha hakuweza kuona kile ambacho Elisha aliona? Macho ya yule kijana katika hali ya nje hayakuwa kipofu, hata hivyo hakuweza kuona kile ambacho bwana wake aliona. Somo hili linahitaji umakini mkubwa na linapaswa kufundishwa kwa muda wa kutosha. Eneo lililomzunguka Nabii lilikuwa limezungushiwa kwa farasi na magari ya moto, lakini hakuna mtu karibu na Elisha aliyeweza kuona katika ulimwengu huu isipokuwa yeye peke yake. Elewa kwamba kwa sababu hauoni haimaanishi kuwa hakipo. Unabii unakuwezesha kuona zaidi ya kile ambacho wengine hawawezi kuona. Unaona mbali na zaidi ya mtazamo wa kawaida wa uhalisia.

Ni ulimwengu wa roho unaoamua matukio ya mwilini. "Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri" (Waebrania 11:3). Elewa kwamba Unabii huona zaidi ya kawaida. Na ninapoamuru na kutangaza kufanikiwa kwako, unapopokea bila mashaka, na mafanikio yatakuwa yako kwa jina la Yesu. Mimi nasema nionayo sio kubahatisha bahatisha .Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Sitatilia shaka Neno la Mungu kama lilivyonenwa na Nabii, kwani najua kwamba Mungu daima huthibitisha neno la mtumishi wake. Mimi ni mshiriki wa wingi wa neema juu ya maisha ya nabii wangu. Kwa hiyo sitahangaika kamwe kwa jina la Yesu. Amina!**

**MASOMO ZAIDI:** Hesabu 22:31




BECOME A GoodNews DAILY PARTNER TODAY BY VISITING
WWW.GOODNEWSWORLD.COM/GNDPARTNER

# GoodNews DAILY
## EVANGELISM





**Matendo 19:15**
**"Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua, na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani?"**

Wana wa Skewa (kiongozi wa kidini) walifikiri wangeweza kufanya kile ambacho Mtume Paulo alikuwa akifanya. Wakristo wengi wanadhani ni rahisi sana kufanya kile mtu wao wa Mungu anafanya, ambayo ni sababu mojawapo inayowafanya wasambaratike na kuunda makanisa yao bila hata utaratibu mzuri. Bila shaka, wengine hustaajabia vyeo hivyo na wangependa kuitwa vyeo hivyo, lakini ukweli ni kwamba, je, umejitayarisha vya kutosha na kuthibitishwa vya kutosha katika Neno la Mungu ili ujiendee peke yako? Ni lazima tuelewe kwamba kuna majemadari na makamanda wa himaya katika ulimwengu wa roho wanaoogopwa na mapepo.

Unahitaji kuwa na tabia ya Yesu ili kukabiliana na mateso na matatizo yanayosababishwa na pepo wachafu. Unahitaji kuwa timamu kiroho na kuelewa jinsi ya kuenenda katika ulimwengu wa roho kabla ya kujaribu vita vya kiroho; la sivyo, ni hatari kwako. Wana wa Skewa wanathibitisha hili. Watu wengi hufikiri kwamba hata unabii ni rahisi, na kila mtu anataka kujiita nabii. Lakini naomba nifafanue kwamba huu si mchezo wa kitoto. Ili kutawala kila shambulio la adui, unahitaji kuwa na msingi katika Neno la Mungu na kuvaa tabia ya Kristo. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mamlaka yangu ni katika Kristo, na nimewezeshwa kutawala na kuwa nuru kwa ulimwengu wa giza. Ninabeba hali ya hewa na kumiliki tabia ya Yesu, na mapepo yanakimbia mbele yangu. Haleluya!**

**MASOMO ZAIDI**
Luka 1:65



**1 Wakorintho 15:58**
**"Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana."**

Paulo aliliandikia Kanisa la Korintho kwamba lisiyumbe katika imani na linapaswa kuwa na mizizi na msingi katika mafundisho yake (Paulo). Ona kwamba Paulo pia aliwatia moyo kwamba chochote wanachomfanyia Bwana si kamwe bure. Mara nyingi, baadhi ya waamini hufikia hatua ambapo wanaanza kutilia shaka uwepo wa Mungu kwa sababu ya msiba kutokea kwa mwanafamilia, mizigo ya kifedha isiyobebeka, au ugonjwa kutoka kwa adui kumharibu mtu wa karibu sana. Katika hali hizi zisizovumilika, swali linazuka akilini mwao, Mungu yuko wapi?

Umewahi kujiuliza swali hili hapo awali? Je, umefika mahali unafikiri Mungu amekutelekeza? Kumbuka kwamba tunapaswa tuwe wa kutoyumbishwa katika uelewa wetu wa Neno la Mungu: chanzo kikuu cha uzima. Mungu hakukufikisha hapa ili kukutelekeza au kukuacha. Yote unayofanya kwa ajili ya huduma sio bure kamwe. Andiko hili linapaswa kuinua imani yako hadi kiwango kingine! Biblia inasema katika (1 Wakorintho 10:13)" Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu, ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo, lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili" . Amina!

## UKIRI WA KINABII

